**JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO**
**SHULE YA SEKONDARI ALFAGEMS (S. 3874)**
**S.L.P. 6083 – Morogoro**
Simu: 0689-783630 (Ofisi Taaluma) / 0685-701614 (Ofisi Uhasibu)
0689-783672 (Bweni la Kike) / 0689-782670 (Bweni la Kiume)
0789-978886 (Airtel Money)
www.alfashule.ac.tz / www.alfagems.com

## TARATIBU ZA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA

Ndugu ........................................................................................., tunafurahi kukujulisha umepata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule yetu iliyoko katika manispaa ya Morogoro, kata ya Tungi, mtaa wa Mji Mwema (kati ya Msamvu na Nanenane). Karibu sana!

Hakuna malipo zaidi ya **ada** ambayo ni:
(a) Kwa mwanafunzi wa kutwa Tsh. 700,000 kwa mwaka.
(b) Kwa mwanafunzi wa bweni Tsh. 1,400,000 kwa mwaka.

Unaruhusiwa kulipa kwa mikupuo minne, yaani Tsh. 175,000 (kutwa), au 350,000 (bweni) kabla ya kila nusu mhula, lakini bila robo hiyo hutapokewa.

Kwa usalama wa wote unaombwa **ulipie benki** (akaunti yenye jina la shule iko CRDB, namba 0152077746000), si kwa mawakala wao wala kwa simu, **halafu vocha uilete shuleni** katika ofisi ya mhasibu upate risiti yetu. Nje ya hapo usitoe pesa kwa yeyote, hata kama ni mwalimu wetu: malipo ya namna hiyo si halali, hivyo shule haihusiki nayo. Jihadhari sana!

Shule imekubaliwa kuwa wakala wa kampuni ya Airtel Money ili kupokea pesa kwa urahisi zaidi. Namba ni 0789-978886 na inatumika pia kwa mawasiliano.

Unapewa siku 35 kulipa ada na kutuletea vocha ya benki au kututumia picha yake kwa Whatsapp (0685-701614); ukichelewa, nafasi yako atapewa mwingine, na wewe utahesabiwa mtu wa akiba hivi kwamba utaweza kupewa nafasi tena tarehe 13-1-2026 alfajiri kama zitakuwepo bado.

Masomo yataanza tarehe **6-1-2026.** Basi:

(a) Ukitaka kuwa mwanafunzi wa kutwa ufike shuleni tarehe hiyo saa 1:15 asubuhi.

(b) Ukitaka kukaa bweni ufike kabla ya saa 10:00 jioni ya tarehe iliyotangulia mwanzo wa masomo (kwa kuwa nafasi hazitoshi kwa wote, watapewa waliowahi kuleta ofisini mwetu vocha ya benki; nafasi zinaweza kwisha hata kabla ya tarehe hiyo).

Ulete Biblia (kama ni Mkristo), kamusi ya Kiingereza, kivuli cha cheti cha kumaliza darasa la saba na vitu vilivyoorodheshwa hapa chini:

1. **Sare** kama ifuatavyo (huruhusiwi kuleta nguo za aina nyingine):

(a) Kwa wasichana:
- (i) Shati jeupe lenye maandishi ya shule
- (ii) Sketi ya rangi ya damu ya mzee (ifikie sentimeta 20 kutoka ardhini)
- (iii) Viatu vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Kwa michezo: fulana yenye maandishi ya shule, trakisuti na raba
- (vii) Masista wanaruhusiwa kuvaa sare ya shirika
- (viii) Waislamu, kwa ombi la mzazi/mlezi, wanaweza wakaruhusiwa kuvaa hijabu halisi nyeupe isiyo na pambo mradi wanyoe nywele zote.

(b) Kwa wavulana:
- (i) Shati jeupe lenye maandishi ya shule
- (ii) Suruali ya rangi ya damu ya mzee
- (iii) Viatu vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Kwa michezo: fulana yenye maandishi ya shule, bukta ya buluu na raba
- (vii) Mabradha wanaruhusiwa kuvaa sare ya shirika.

2. Kwa kukaa **bweni**:
- (a) Fulana ya kijani yenye maandishi ya shule
- (b) Nguo ya kulalia na ya kwenda bafuni
- (c) Mashuka na blanketi
- (d) Chandarua kilichotiwa dawa
- (e) Godoro la futi mbili unusu
- (f) Ndoo
- (g) Sanduku imara na salama
- (h) Taulo na vifaa vingine vya usafi
- (i) Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
- (j) Nauli ya kurudi nyumbani wakati wowote (ukibaki wakati wa likizo utalipa Tsh. 2,000 kwa siku).

**N.B. Ni lazima** mashati, fulana za shule, sketi, suruali na sweta vinunuliwe shuleni.

Biblia (Tsh. 22,000), kamusi (Tsh. 22,000), magodoro (Tsh. 42,000), mablanketi (Tsh. 15,000), mashuka (Tsh. 7,000), vyandarua (Tsh. 6,000), trakisuti (Tsh. 20,000), taulo (Tsh. 6,000), ndoo (Tsh. 4,000), begi (Tsh. 20,000), viatu (Tsh. 30,000 visipozidi namba 39, Tsh. 38,000 namba 40-42), madaftari na kalamu vinapatikana shuleni kwa bei nafuu kama ilivyoonyeshwa katika mabano.